

## GOMBO LA ISIMU TUMI

**NI KUFUWATA SATI ZA MAJAGINA WA ISIMU**

**DKT. MOHAMED KARAMA, UNIVERSITY OF KABIANGA**

Mapitioyo: **Mikondo ya Kiswahili: Siasa, jamii na utandawazi**, Alamin Mazrui na Kimani Njogu, Twaweza Communications & The Red Sea Press, 2022, kur. 192, KSH 900 (jalađalaini)  
ISBN 978-9966-128-07-2

Kazi hii ina sehemu mbili k<sup>b</sup>uu: Sehemu ya kanza ‘inayojishughulisha na maendeleo na mabadiliko ya kiisimu ya lugha ya Kiswahili kutokana na changamoto mpya zilizokikabili hivi leo’ (uk. xv); na sehemu ya pili inayokiyangaliya kiSwahili katika mawañda mapana ya umaeneyo na unavojikifu katika ulimengu mpya wa utanrawazi. Kiisimu waanđiši wanaangaziya umuhimu wa tafsiri katika muktađ'a wa uṭawala wa kikoloni, māmko wa wanaṭi wa kiSwahili d'iđi ya kiSwahili ča kupawa na namna kiSwahili kinavoweza kujifunza kuṭokana na juhuđi za luğha nyengine za ulimenguni—kiArabu, kiJaponi, kiTuruki, kiMandarini katika keleza haliya za kisanyansi na kiteknolojiya ya kisasa na uwezekano wa kukiboreša kiSwahili kelezeya mawañda hayo. Hali kađalika, Ukaṭiba na utekelezaji wa vipengele vake ikiwa ni mahakamani au bungeni na čangamoto zilizoko katika utekelezaji huwo piya zinačangiya katika kuṭafuta suluhišo la kuwapa wananci haki yao bila pingamizi za kiisimu. Mikakati hii mipya ya kukiyenreleza kiSwahili wanayoipendekeza waanđiši hawa, nami nakubaliyana nawo ka kiwango fulani, ni matumizi zaiđi ya tafsiri stahikifu. Wameona tafsiri itasaiđiya kuleta upya wenye natija katika uṭamađuni wa mSwahili na kuwafanya wageuze ṭaaluma hizo kukid'i mahițaji ya mSwahili na mAfrika katika Karne ya 21. Kisisi, tafsiri ni njiya mojawapo za kukikuza kiSwahili lakini kisiyegemewe sana, kiṭafifiza ubunifu wa nrani wa kutunga kwa kiSwahili.

Umajumuwi unawoangaziwa katika sehemu ya pili unaanziya ‘nyumbani’ kenyé Jumuiya ya Afrika Mašariki. Ka kujifunza kuṭoka nči za Mağaribi na Jumuiya yao ya Bara Ulaya walipojivuwa kuṭoka ukoloni wa kuṭawaliwa na waRumi, halafu kujenga usthaarabu wao wenyewe na haṭimaye kujikimu ka ḱenreleza čumi zao ni funzo Jumuiya ya Afrika Mašariki inaambiwa iliṭaye. Katika mipangiliyo hii yoṭhe wanaṣađidiya kiSwahili kiweke kati na kati na kiwe nričo čombo ča kuleta ufanisi huwo. Kanziya masokoni, vyuwoni, na viwanrani (ka kupokeya teknolojiya inayostahili) kiSwahili kiimarišwe na kipawe umbele. Lakini zaiđi, ni kukubali uwingu wetu na kamba uhuru wa kutega učumi usikinge na mipaka ya kiyuṭaifa baina ya wat<sup>h</sup>u na wat<sup>h</sup>u au nči na nči. Na haya ya umajumuwi wa kimaeneo kutumiya luğha moja ulišajaribiwa ka kanzišwa luğha ya kiAfrihili (umahuluti wa ki-Afrika+Swahili), luğha iliyotarajiwa kuwa luğha ya Bara Afrika. Ijapokuwa luğha hii haikupata msukumo wala motiša kuṭoka serikali za Afrika wala watumiyaji wake, basi ipo haja ya kangaliya ṭena swala hili la luğha ya Afrika minṭarafu ya kiSwahili maana ulimengu sasa ni wa kujipanga kimaeneo na kufaidika kiđarahima. Waandiši hawa wanabainiša kuwa luğha iliyoko “masokoni” nriyo luğha ili(ṭa)yofauliša Učumi wa nči (uk. 91—92) na utumiyaji wa luğha hii ya mawasiliyano mapana huweza kuleta natija katika sekta nyenginezo kama ya Sayansi kwa kwenrelezwa “uṭamaduni wa sayansi” badala ya “ujuzi wa sayansi” (uk. 93). Yaani kuifahamiša elimu ya sayansi kwa wananci wa kawaida mašinani.

Katika Utangulizi kunafafanuliwa makuzi ya kiSwahili, na sababu zilizopelekeya upanuzi huwo zikiwamo: biyašara, elimu, umišinari, vita, na kukuwa ka miji mikuba na suwala la ufanyakazi unawoanđamana na uhamiyaji yaliṭafsiliwa. Mkusanyiko huu wa wat<sup>h</sup>u ainaṭi na luğha zaOo na siyasa inayoañdamana nayo, kimaoni yetu, limezuwa suwala la ‘Kiswahili kinahesabiwa ni lugha ya Kibantu’ (uk. ix). Taaluma ya Isimu ya kiBantu inakingeliša kiSwahili kuwa luğha ya kiBantu na waanđiši hawa hawaelezi msimamo wao kuhusu ḫana ṭaşwiši ya ‘kinahesabiwa’. Aid'an, waanđiši wametumiya, si kiAn'roplojiya, ‘waswahili’ (uk. xi, xvi, 6, 7) au ka kusositiza, ‘waswahili wenyewe’ (uk. xvi, 50, 53), au ‘Uswahilini’ (uk. 16) ka maana ya

‘wenyeji wa Mwambao wa Pwani ya Afrika Mashariki’ (uk. xi) lakini katika Sura ya Tatū ‘istilahi’ hii inayepuka kelezwa waziwazi bali kunatelewa maelezo ya nani hakujumuišwa kuwa ‘mswahili’ (uk. 50-51), kiličolakabišwa ‘kipwani’ (kisermačo eneo la Maili Kumi uk. 52). Je, mSwahili ni nani na luğa zao ‘[zinazo]zungumzwa na iğadi ndogo ndogo’ (uk. x) haziwezi kutambulišwa kupitiya ufanuzi wao wa ‘itikadi’ (uk. 43) na ‘utamaduni’ (uk. 76)? Ni kitenrawili waličowačiwa wasomaji wajijibu maana maswala ya ‘ujitambulishaji’ (uk. 81), japo una faida, waweba kuleta ‘ubeberu’ (uk. 95), kimaoni yubo. Yaonekana waanđiši hawa waličafilika na makala ya ms̄taafu Rais Uhuru Kenyatta kenyē Baraza la Usalama la Umoja wa Mařaifa alipoangaza kuwa asili ya mizozo inayošuhudiwa sasa ulimenguni imesababišwa na utambulišo (Mutambo, 2021). Msamiači huu ‘waswahili’ hauwonekani tēna baađa ya Sura ya Tatū ka sababu sura zinazofuwata, japo zazungumziya ‘utambulišo’ katika rasa ya kiAfrika, lakini yajikita zaiđi katika luğa kuliko wat<sup>h</sup>u.

Kufu na anwanitoto ya kazi hii, ‘siyasa’ yaonekana nriyo iliyowašuguliša zaiđi waanđiši. Sura ya Siňa inajikita katika kufanuwa siyasa ya kujipanga kimaeneo na kukipa kiSwahili uwezo mkubwa kupambana na hali mpya ya Mpango Mpya wa Ulimengu unawotiliya maanani utanrawazi (mařifa ya Mařaribi kufađika zaiđi) na badiliko la hewa kupiga Mařariki baăda ya Vita Bariđi va kale (Amerika vs Russia) kumalizika na vita bariđi vypa (Mařaribi vs urafiki wa China & Russia) kuzuka. Lakini swala wazi katika mčakato huu mzima ni kamba kiSwahili hakimo katika mahesabu ya mivutano ya ‘ñđovu’ hawa wa kiyučumi. Amerika inajipanga upya ka kujinguvuza—kujifikirya wao kanza katika masiyala yoyoč<sup>h</sup>e: kiyučumi, kisiyasa na haťa kijamii—na China na Russia zina luğa zao ambazo wataka zisambaye ili atari zao zipatikane kila wanapokita mizizi yao. Waanđiši hawa kenyē masimilizi haya ya kisiyasa, učanganuzi wao umegawa makunri ya watumiyaji kiSwahili katika mařabaka kulingana na itiķadi ya kiMaksi (uk. xi, 26, 145, 146). Mgawo huu wa kitabaka wafahamika ka sababu, pengine, ni kutočana na kazi zao za awali Mazrui (1982) na Njogu (1987). Ka hivo, hivi sasa, je, makuzi ya kiSwahili yamenasibišwa na ‘wageni wanavokičukuliya’ (kur. 131 - 135) na kamba ‘umataifa’ wa kiSwahili ni ‘sarabi’ kani luğa yenyē ‘nguvu’ yategemeya nguvu za kiyučumi, au kutokee vita vengine kama wanavomaka waanđiši wenywē (uk. 141)? Tarakibu yao kuhusu luğa ni kukifanya kiSwahili kikimu na kitimize mahitaji ya watumiyaji wake wa nrani yaani waSwahili—jamii ka maana ya kiisimujamii—wa eneo la Afrika Mařariki.

Utafiči na uwasišaji wa kazi hii ulikuwa wa kurid'iša. Haťa hivo, katika kazi nzima kuna madonro makubwa ambayo yalihičaji yatafsiriwe na yaločukuwa nafasi kubwa ambayo ingefaa kangaziwa hoja muhimu zilizokosekana kama: luğa za kijamii zinavoweza kukikuza kiSwahili ka kujihusiša na ċuwara la kiSanifu; utať'mini wa kiSwahili katika manħaji mpya ya Utentraji (CBC) huku Kenya, japo, wameeleza kuhusu Tanzania kulegeza kamba katika ufunzaji ka kiSwahili (uk. 118) au Afrika Kusini inavojizađi kukiweka kiSwahili maskulini (uk. 113); juhuđi za kenrelezwu kiSwahili na BAKITA, BAKIZA, BATAKIKE (hawakulitaja kamba imepita miyaka mitatu na bađo baraza hili halijaunrwu ncini Kenya) ni taasisi ambazo hazikutajwa karne matinini lakini walijoneša sikitiko kuwa hakuna čama kilokisukuma Afrihili (uk. 106); tukiylo la kihistoriya la tangaavu la COVID 19 liliovařiri kiSwahili halikutajwa japo kuna data mpya za 2021 (uk. 143); na haťa masiyala mapya ya Wekevu Bune (AI) na kiSwahili hayakušuġulikiwa; ‘Laana ya luğa nydingi’ (uk. 100) ni swala la utambulišo ambapo wenye luğa za kijamii za kiSwahili wanapiganija kutotengwa juu ya ukatiđi wao (Mberia, 2016) halikufafanuliwa bali kuwačiwa bišara (uk.57). Japo kuna Kiyambatišo ča kutambuliwa ka Siku ya Luġa ya Kiswahili Duniyani lakini suwala zito kama hili limepawa ibara mbili—kama tarifa tu wala si mjađala—katika ukurasa wa mišo wa kitabu hiči. Iličarajwa kuwe na mtinro mmoja wa uwaanđiši wa majina ya luġa ka mfano: KiJerumanī, KiRomansi, KiSlavi (uk. 5), KiMandarin (uk. 20), KiDomari, KiNobiin, KiBedawi (uk. 99) tafauṭi na Kiswahili (moč<sup>h</sup>e kitabuni), Kitikuu (Kibajuni); Kipate; Kisiu; Kiamu; Kimvita; Kingare n.k (uk. 50). Ka kutumika ‘kihitimisho’ katika kila sura ilikuwa ni d'ämira ya kutafauṭiwa na sura ya mišo ‘Hitimišo’ kufuwatiša mtinro wa Pwani University kenyē uwaanđiši wa tasnifu za Uzamili na Uzamifu, lakini ikađidka ‘kihitimisho’ (uk. 145), labda ka kučafilika.

Kazi hii ni ya kisasa na mjađala iliyoangaziwa ni muhimu katika maenreleo ya kiSwahili. Yaſtahiki kusorňa ni yoyoč<sup>h</sup>e: msomi, mtafiči wa kiSwahili, au msomaji wa kiburuđani.

## **Marejleo**

Mazrui, A. (1982). *Kilio cha haki*. Nairobi. Longman.

wa Mberia, K. (2016). "Mother tongue as media of instruction: The Case of Kenya" katika *The University of Nairobi Journal of Language and Linguistics*, 5, 46-59.

Mutambo, A. (2021, October 12). Uhuru at UN: Kenya says identity politics a ticking time bomb.  
Imesomia: <https://nation.africa/kenya/news/uhuru-at-un-kenya-says-identity-politics-a-ticking-time-bomb-3580204>

Njogu, K. (1987). *Maudhui ya mapinduzi katika riwaya za kisiwani Zanzibar*. T̄asnifu ya Uzamili, Čuo Kik<sup>h</sup>uu ča Nairobi, Nairobi.

## **Imepitiwa na:**

Mohamed Karama  
Idara ya Isimu Fasihi na Mawasiliyano  
University of Kabianga  
Keričo, Kenya.

**Šukurani:** Asanṭa k<sup>h</sup>uu imenree msomaji-pofu wa makala haya wa Jariđa t̄ajika ḁa maoni yaloiboreša t̄ahakiki hii.

**Kauli Mtakaso:** Maelezo yaliyomo humu ni yangu na si ya UoK wala Idara yetu. ḁa lolot<sup>h</sup>e kuhusu makala haya na/au Elimu ḁa jumla wasiliyana nami [mkarama@kabianga.ac.ke](mailto:mkarama@kabianga.ac.ke).